


# KIJASHO CHEMBAMBA

Na: Richard MWAMBE

©Jamvi la Simulizi 2025

## Ilipoishia

***Tayari akili ya Madam S ilikwishaanza kuchakata mambo juu ya hilo. Akiwa bado anamsikiliza Inspekta, simu yake ikaita kwa fujo. "Kumekucha!" akasema mara baada ya kuona 'Kitala' likisomeka. Alihifadhi namba ya Rais kwa neno 'Kitala'.***

***"HOT" akaitika.***

***"Fika kilingeni haraka!" sauti ya upande wa pili ikamwwamabia na simu ikakatika. Madam S akainuka na kumtazama mzee huyo aliyekuwa mbele yake.***

***"Nitakutafuta…" akamwambia.***

***"All the best Selina!" Simbeye akatamka. Madam S akaondoka ndani ya mkahawa ule. Haikuchukua hata dakika tano na Inspekata Simbeye naye akaondoka zake.***

## Endelea…

✠ ✠ ✠

Ndani ya ofisi muhimu ambayo mheshimiwa Rais hufanya mikutano ya siri na watu wake muhimu, alikuwa akizunguka huku na huko. Moja haikai wala mbili haikai. Alitoka kona hii akaelekea ile kule. Tangu aingie hapo tayari pakiti moja la sigara aina ya Sportsman lilikwishateketea. Hodi iliyobishwa kwa utulivu ilimrudishia uhai ambao uliondoka kwa sekunde kadhaa zilizopita. Msaidizi wake akafungua mlango na mwanamke mtu mzima akaingia ndani ya ofisi ile. Mheshimiwa Rais akaitazama saa yake ya mkononi na kutikisa kichwa juu chini.

“Keti!” alimwambia mgemi wake huku naye akikiendea kiti chake na kuketi pia. “Selina! Nashukuru umekuja kwa wakati,” akamwambia na wakati huo yule mhudumu alikuwa nje ya chumba hicho.

“Naam nimeitikia wito,” Madam S akajibu.

“Tumeibiwa kitu muhimu sana… na cha siri mno!” akaongea huku akifikicha macho yake. “Kokwa! Kokwa hakikuwa kitu cha kimaonesho lakini ilionekana kuwa ndiyo njia pekee ya kukihifadhi,” akasema.

“Nakuelewa mkuu, lakini naona kama habari yenyewe unaianzia katikati…” Madam S akamwambia.

“Doh shit! Akili yangu yote nilifikiri naongea na ADC. Ni hivi, kuna wizi umetokea usiku wa kuamkia leo pale jengo la makumbusho…”

“Ndiyo!”

“Kimeibwa kitu muhimu sana katika nchi yetu ambacho kwacho serikali inaweza kuendesha mitambo yote ya nyuklia iliyosimikwa katika machimbo yetu huko Bahi na Namtumbo…” akaeleza.

“Ndiyo mkuu…” Madam S akazidi kusikiliza.

“Unajua kuwa baada ya ugunduzi wa madini haya hadimu nchini kwetu, tuliingia mkataba na Rusia na China ili kufanya uchimbai wa awali. Na tulipojiridhisha basi tuliwapa kibali cha kuyachimba kwa mkataba maalum ambao sina haja ya kuuzungumzia. Najua unaujua vyema kabisa…” Rais akazunguma.

“Ndiyo najua hayo yote,” Madam akaitikia.

“Sasa baada ya miaka hii yote, tuliingia mkataba mwingine na wanasayansi hao wa Urusi ili kurutubisha kiasi kidogo cha

madini hayo na kutengeneza silaha ambazo kwazo tungeweza kufanya biashara au kutumia kwa kujilinda dhidi ya vitisho vya mabeberu. Lakini tukajenga mtambo mkubwa wa kufua umeme kule Bahi, Dodoma. Umeme ule unaotoka katika kile kinu ni mkubwa sana, tumeuza nishati kwenye nchi zote zinazotuzunguka… nielewe, nchi zote. Hapa kwetu mtandao wote wa SGR unatumia nishati ile, viwanja vya ndege vyote nchini vimeunganisha na nishati ile, na kwa wateja wetu yaani majirani nao wote wameunganisha miundo mbinu muhimu kupitia kinu cha Bahi…" akanyamaza kimya kwa sekunde kadhaa, kisha akainua uso na kuendelea, "Sasa ile kokwa ina mfumo ambao unaweza kuuzima ule mtambo muda wowote. Na ukiweza kuuzima maana yake frika Mashariki yote itapata hitilafu za uendeshaji katika miundombinu yao muhimu. SGR zitasimama, ndege hazitaruka maana mifumo ya ardhini ya kuongozea haitafanya kazi na kadharika. Lakini pia mfumo wa makombora ambayo tunayo pia upo mule, kuyaruhusu yafanye maangamizi au la, kila kitu kipo mle. Kwa kifaa kile unaweza kuilipua nchi yote ya Tanzania within one second, na Afrika itakatika katikati… na mambo mengine mengi…" akaongea kwa uchungu. Hapo Madam S akagundua kwanini Rais kachanganyikiwa namna hiyo. Naye akiwa katika kuwaza hilo akahizi kitu kimewekwa mezani, mbele yake tu. Alipoinua uso, akakutana na kabrasha lenye ukubwa wa wastani.

"Chukua hilo faili… ni faili la siri sana kama lilivoandikwa hapo juu "Top Secret", nenda ukalipitie kwanza, nakupa saa ishirini na nne. Ukishamaliza na kunote vitu vya msingi unirudishie hapa.

"Sawa mkuu… je unataka idara yangu iingie kazini katika sakata hili? Maana mwanzoni hatukuona kama lina hadhi yetu kwa kuwa tulijua wazi kuwa kokwa ni sehemu tu ya maonesho kwa wageni," Madam S akazungumza kwa tuo.

"Mliona na wengine waliona hivyo pia… si kila mtu anajua kokwa ni nini… ni watanzania wasiozidi wanne wanaojua siri ya kile kidude, by the way…" akachukua sigara nyingine na kuiweka kinywani kwa kuibana kwa papi mbili za midomo yake. Akawasha kiberiti cha gesi na kuipa moto. Akapiga pafu mbili za maana na kuuwacha ule moshi usambae hewani kwa madaha… "kasome hilo jalada, utaona kila kitu. Haruhusiwi mtu yeyote kugusa hilo kabrasha tafadhali," akamalizia kusema. Mwanamama yule alilichukua kabrasha lile mikononi mwake huku kijasho chembamba kikimtiririka. *Jambo zito!* Akawaza.

"Sawa mkuu!" Madam S akasimama na kutoa heshima ya kijeshi, kisha akaongoza na kutoka nje ya ofisi ile.

## SURA YA 2

DANI ya Ofisi Ndogo, ilikwishapita saa ya tano tangu ℕmwanamama huyo aketi kulisoma jalada lile. Pembeni yake palikuwa na kijitabu kidogo alichotumia kunakili kando mambo kadhaa aliyoona ni ya muhimu kwake katika utendaji wa shauri hilo. Wapi ni muhimu kufika, nani anapaswa kuhojiwa na nani anapaswa kuchunguzwa, nani anapaswa kuuawa nan i anapaswa kufufuliwa kutoka wafu; yote hayo alikuwa akiyanakili kutoka kwenye lile kabrasha. Aliamini atapata mwanzo mzuri katika utafiti huo.

Kabrasha lile lilikuwa zito, si kwa uzani bali kwa kile kilichoandikwa kwa mshine baridi. Picha kadhaa zilizopigwa kwa kamera ya kizamani ziliweka kumbukumbu isiyofutika katika karatasi zake. Alipohakikisha ameweka kando mambo ya msingi ya kufanya na watu wa msingi wa kufuatilia ili kujua hili na lile, pia akaweka na maswali ya kuwahoji watu hao na nini cha kwenda tazama katika sehemu alizozichagua. Akafunga kabrasha lile na kulitia kwenye saraka yake ya siri amabyo ni yeye tu awezaye kuifungua. Na hata kama jengo litawaka moto lakini saraka hiyo haiwezi kuteketea kutokana na malighafi iliyotumika kutengeneza. Akasogeza simu yake na kubofya tarakimbu kadhaa ili kukamilisha ile namba anayoitaka. Alipokamilisha akaweka mkonga karibu na sikio na kutulia.

Upande wa pili, simu ilipokelewa na Inspekta Simbeye. Kwa sauti ya utulivu alizungumza na mwanamama huyo na kuweka miadi ya kukutana naye jioni alasiri ya siku hiyohiyo.

*"Nafikiri mgahawa wa Salamanda patakuwa pazuri zaidi…"* Simbeye akamwambia Madam S.

"Sawa, saa moja ijayo!" wakakubaliana.

Ghafla, siku ilikuwa fupi kwa mwanamke huyu jasusi aliyekubuhu. Aliinuka kitini na kutazama nje kupitia dirisha kubwa lililo ofisini kwake. Mienendo ya wananchi ilikuwa ikiendelea pasi na papara yoyote. Hakuna hata mmoja kati yao aliyekuwa akijua nchi inapita katika wakati gani. Ni wachache tu waliokuwa wakifikiri nini cha kufanya ili mambo yakae sawa. Akajiweka vizuri na kuufuata mlango. Dakika mbili zilizofuata, alikuwa barabarani akitembea kwa miguu yake miwili ili kuufikia huo mgahawa wa Salamanda. Lakini ghafla, tukio hasilolitegemea lilitokea. Kijana mmoja aliyekuwa katika uelekeo sambamba nay eye alimpiga kikumbo cha nguvu. Madam S akapoteza uzani na kuyumba kuelekea barabarani. Sekunde hiyohiyo gar aina ya Subaru lilitokea nyuma yake kwa kasi na kumgonga vibaya. Mwanamke yule akaangukia katikati ya barabara akigalagala kwa maumivu. Kelele za wapitia njia zilisikika na kuvuta hisia za watu. Subaru lile lilipotaka kusimama watu wakalivamia, dereva akaliondoa kwa nguvu na kugonga wengine wawili kisha akatokomea zake. Madam S akiwa anavuja damu akabebwa na wasamalia wema na kumpakia kwenye gari jingine, safari hospitalini ikaanza.

✠ ✠ ✠

Simu ya Kamanda Amata iliyokuwa kwenye meza ndani ya chumba cha hoteli iliita kwa fujo. Si kwamba hakuisikia bali aliipuzia. Uchovu na kazi za mchana kutwa vilimfanya mwanaume huyo kulala kama mtoto. Ilirudia kuita na kuita, hakuichukua haraka kwa sababu ilikuwa simu ya marafiki. Haikuwa ile simu ya taarifa nyeti za kiofisi. Lakini ilipomkera zaidi, aliinua mkono wake na kuinyakuwa. *'Inspekta'* ilisomeka. Akili ya Amata ikakaa sawa. *Siyo kawaida huyu mzee kunipigia simu*

*mfululizo namna hii!* Akawaza. Akaketi vizuri na kuanza kubofya ile namba. Lakini kabla hata hajamaliza ikaanza kuita tena.

"Inspekta!" akaita.

*"Kamanda, upo wapi?"* Inspekta Simbeye aliongea kwa sauti ya upole. Sauti ambayo ilimshtua Amata.

"Nipo Arusha… vipi mzee unaumwa?" Amata akauliza kwa mashaka.

*"Hapana, ila fanya unaloweza leo hii ufike Dar es salaam, kuna jambo zito sana…"* Simbeye akamwambia Amata. Amata akabaki kimya hakujibu kitu mpaka ile simu ilipokatika. Kabla hata hajajiweka sawa, simu yake nyingine ikaita. Hiyo aliijua moja kwa moja ni ya nani. Gina! Akaichukua na kuiweka sikioni.

*"Amata, Amaaaaata, Madam S ana hali mbaya sana, wahi tafadhali*," Gina aliongea harakaharaka huku akilia.

"Tulia Gina, unajua taaluma yako vizuri, hutakiwi kuwa mtepetevu namna hiyo… ukianza kulia wewe na wengine wafanye nini? Haya nakuja, hakikisha umeweka usalama wa kutosha dhidi ya Madam S, usiruhusu mtu yeyote amuone wala amtibie isipokuwa Daktari Jasmini na ikiwezekana muhamishieni Mzena, nipo njiani nakuja!" akampa maelekezo na kukata simu. Amata akashusha pumzi. *Nini kimempata mama huyu?* Akajiuliza. Hakujiuliza mara mbili, hata kama alikuwa na miadi na mrembo Leonara, moyoni mwake alijisemea tu 'atanisamehe'. Akapanga vitu vyake kwe ye mkoba na kukatisha kile alichokuwa akikifanya jijini hapo na kuondoka zake.

Katika uwanja wa ndege wa Arusha alibahatika kupata ndege moja ya kukodi na kuitaka imfikishe haraka jiji Dar es salaam. Tayari alikwishawaweka sawa watu wake wote wa TSA, maana kadiri ya hiarakia ya kazi ndani ya ofisi yao ni kwamba

ikitokea HOT ambaye ndiye Madam S yupo katika hali ya kutoweza kutoa maamuzi yoyote basi TSA 1 anakuwa na jukumu hilo mpaka Rais atakapoteua mwingine kwa siri. Hivyo Kamanda Amata, mara moja alikwishachuku jukumu lake. Ndani ya ndege ile aina ya Sessina alikuwa peke yake na mawazo yake lukuki. Mhudumu alipomjia ili amhudumie kinywaji, hakutaka kabisa na aliomba awe peke yake bila bugudha. Kijasho chembamba kilikuwa kikimteremk kila alipojiuliza nini kimempata mwanamama huyo ambaye kwake ni boss, mwalimu, mzazi na mkufunzi.

**Dar es salaam**
**12:05 Jioni**

Jiji la Dar es salaam lilimpokea Amata jioni hiyo. Katika uwanja wa ndege wa Mwalimu Julius Nyerere, terminal ya kwanza, Gina alikuwa hapo tayari kumpokea bosi wake. Aliliacha jengo lile na kutoka nje kabisa kuelekea kwenye magari ya kukodi. Lakini ghafla alisikia mbinja iliyopigwa kiufundi kabisa. Aliitambua. Na alimtambua mpigaji. Akabadili uelekeo na kulifuata gari ambalo tayari alikwishaliona lilipoegeshwa. Akaingia na kuketi kwa utulivu huku akionekana kusawajika kwa mawazo.

"Amata!" Gina akaita. Amata akageuka kumtazama mwanamke huyo, "Vipi, mbona una mawazo mengi?"

"Swala la Madam S limenivuruga kidogo… amepatwa na nini?" akauhoji.

"Amepata ajali," Gina akajibu.

“Ajali? Ajali!” Amata akatamka na kubaki kimya. Alijuwa wazi kabisa nini maana ya ajali kwa mwanamama kama yule. “Ameanguka na gari au imekuwaje?”

“Amegongwa na gari… nilipita eneo lile kusikiliza wambea… inasemekana amegongwa na gari lakini lile gari halikusimama,” Gina akaeleza. Amata akatikisa kichwa juu chini kuonesha sasa akili yake inafunguka taratibu.

“Eneo gani?” akauliza.

“Mtaa wa Samora… alikuwa akitoka. Inaonekana alikuwa akitoka ofisi ndogo lakini sijui alikuwa akielekea wapi,” Gina akaeleza wakiwa bado palepale kwenye maegesho ya uwanja wa ndege.

“Simu zake…”

“Hatukuzipata hivyo nilimpa taarifa Chiba na amenihakikishia ameshafanya kazi yake,” Gina akaeleza huku akiwasha gari na kuliondoa eneo lile. Amata akashusha pumzi ndefu na kugonga ngumi kwenye dashboard ya lile gari.

“Kuna kitu… siyo bure! We unafikiri itakuwa ajali kama ajali?” Amata akamtupia swali Gina.

“Sijajua mpaka sasa, nilikuwa najaribu kudodosa huku na huko lakini sijajua kama kuna jambo jingine au la ni maadui zetu wanaotuwinda siku zote,” Gina akaeleza.

“Ni kweli!” Amata akajibu na kuinua simu yake, akabofya tarakimu kadhaa na kuiweka sikioni.

“Nimefika jijini mzee,” akazungumza na mtu wa upande wa pili. Sekunde kumi baadae akakata simu na kumgeukia Gina. “Nipeleke Oysterbay Police, uniache hapo…” akamwambia. Gina akakubali na kuongeza kasi ya lile gari kuelekea huko

alikoambiwa. Iliwachukua dakika thelathini na mbili kufika polisi Oysterbay.

“Nitakupigia baadae tuonane mahali… we niache hapa kaendelee na shughuli nyingine,” Amata akamwambia Gina. Gina akaondosha gari na kumwacha Amata kasimama palepale jirani na lango la kuingilia katika kota za polisi. Alipojiridhisha na kile alichokuwa akikitazama, akavuta hatua na kuzipita nyumba kadhaa zilizochoka. *Sijui kwanini serikali haiwapi mazingira bora polisi. Namna hii wataacha kupokea rushwa kweli!* Akawaza. Amata alizipita nyumba kadhaa huku akisalimia kila anayekutana naye. Muda huo ni watoto na wanawake waliokuwa vibarazani wakiendelea na shughuli mbalimbali. Hakujali macho yaliyokuwa yakimsindikiza, yeye alisalimi na kupokea salamu basi. Alipoufikia mlango anaoutaka hakugonga hodi, alinyonga kitasa na kuingia ndani.

“Karibu sana!” sauti nzito ya Inspekta Simbeye ilimkaribisha huku mzee huyo akiinuka kitini alipokuwa ameketi na kitabu chake cha Operesheni Kashmir. Akapeana mkono na mgeni wake.

“Asante nimefika…” Amata akaitikia.

“Keti bwana… keti kabisa upumzike. Najua una mawazo mengi kichwani lakini usihofu…” Simbeye akamwambia Amata huku akiliendea jokofu lake na kutoa pombe kali, “Leo nina hii bwana, hebu kunywa ikutoe nishai kidogo!” akamwambia huku akiitua chupa kubwa ya John Walker mezani na kisha akaleta tonic soda. Akaingia jikoni na kutoka na kibakuri kilichojaa viapande vya barafu na kingine kikiwa na malimao kadhaa. Amta hakusubiri, akajimiminia kwa kipimo chake, kishapo

akatumbukiza barafu na kipande cha limao, akaviacha humo vizoeane.

“Nipe habatri mzee… maana nimeona hapa ndipo pa kuanzia,” Amata akatamka huku akijiweka sawa kitini.

“Mama yako amegongwa na gari…”

“Najua!”

“Sawa… sasa nilikuita, na siyo kawaida na wala sitakiwi kukuita ila niliona unapswa kuwa hapa karibu na mama yako. Unajua ninyi mna maadui wengi sana wa ndani na wa nje ya nchi…” Simbeye akasema. Amata akajibu kwa kichwa. “Sasa hatuwezi kujua, ni ajali kama zingine au kuna jambo nyuma yake ukizingatia sijui mna jalada gani mezani penu,” akaongeza kusema. Amata alibaki kimya kabisa.

“Umemuona tangu apate ajali?” akauliza.

“Ndiyo!”

“Umezungumza naye?”

“Hapana, hana fahamu kabisa…” Simbeye akamwambia Amata.

“Sawa! Kama hana fahamu ni jambo jema…” Amata akasema na huku akiinua bilauri yake, akapiga mafunda mawili ya kile kinywaji, akakisikilizia kikiwa kinashuka taratibu kooni pake.

“Mhm!” Simbeye akacheka kwa mguno, “sina la kukuhoji maana akili yako daima huwa inatangumia mamilioni ya kilomita za kimawazo… kwanini unasema ni jambo jema?”

“Ili watu wasimsumbue kwa maswali…”

“Ok! Hapo nimekuelewa. Si unaona sasa, wakati mimi nilikuwa nasema kwanini kapoteza fahamu,” Simbeye akamwambia Amata. “Sasa Kamanda nitakupa doti moja halafu

wewe utaona uanzie wapi… kuna jambo limetokea hapa usiku wa kuamkia leo…”

“Unamaanisha nini?”

“Unajua Kokwa?” Simbeye akamuuliza Amata.

“Si ni hii teknolojia walioitangaza hawa wanasayansi wa Urusi ambayo wameitengeneza kwa ushirikiano na wataalamu wetu wa ndani…” Amata akaeleza.

“Ewaaaaaa…”

“Naijua, si unajua data muhimu kama hizi lazima ziwe miezani petu kwa usalama wa nchi!” Amata akaeleza huku akipiga funda jingine.

“Sawasawa… sasa jana mchana palikuwa na tafrija ya kuizindua hapo kwenye ukumbi wa Makumbusho ya Taifa…” Simbeye akasema.

“Ndiyo nafahamu, na nilikuwa na kadi ya mwaliko sema ndo hivyo nilikuwa Arusha,” akamjibu.

“Dah!” Simbeye akasita kuongea.

“Kimetokea nini?” Amata akahoji kwa shauku huku akiitua bilauri yake mezani. Tayari aliyasoma mawazo ya mzee huyo.

“Ile rimoti, kokwa, imeibwa usiku wa kuamkia leo, palepale Makumbusho!”

“Mtumeeeeee!” Amata akajikuta akitaja jina la Mtume pasi na kutarajia.

“Imeibwa na mpaka sasa hakuna hata fununu ya ilikuwaje… sasa nilikuwa na mama yako majira ya saa tano hivi asubuhi, nikampa taarifa hizi. Na tulipokuwa tukiongea akapigiwa simu, of coz sijui ilitoka wapi, tukaagana akaondoka. Muda wa saa tisa hivi akanipigia tuonane pale Salamanda, sasa nafikiri akiwa njiani ndiyo hilo jambo likamkuta…” Simbeye akamweleza Amata.

Ukimya ukatawala kati yao. Amata akasuuza koo kwa kikoozi uchwara, akatikisa kichwa chake taratibu juu-chini.

"Inspekta, unafikiri hilo jambo ulilonimbia na hiyo ajali vinaweza kuwa na uhusiano fulani?" akauliza.

"Siwezi kusema ndiyo moja kwa moja, na ndiyo maana nilikupigia ili tuonane kabla hujakutana na mwingine yeyote… labda kwa hili unaweza kupata pa kuanzia…" Simbeye akamwambia Amata huku akiinua ile chupa ya John Walker na kummiminia tena ile pombe kali, "najua ukipata hii na akili inarudi…" akasema wakati anarudishia kizibo cha ile chupa. "Sikia kijana, hapa kuna jambo zito hasa kwenye hili suala la kokwa, isije kuwa ndiyo mambo yameanza…" akamwambia.

"Halitakuwa zito la kushindwa kulibeba, mangapi tumeyapatia ufumbuzi sembuse hili?" Amata akajibu na kuinua ile bilauli akajimiminia yote kinywani, "mzee… naenda nitakupigia kesho au kama itatokea dharula," akamuaga huku tayari keshainuka kutoka pale kitini.

"Be carefull kijana, unajua kuwa taifa linakutegemea…" Simbeye akamwambia Amata huku akimpigapiga begani.

✠ ✠ ✠

Amata alipoiacha nyumba ya Inspekta Simbeye, usiku uleule alielekea ofisi ndogo. Kichwani mwake alishajiwekea tahadhari kubwa kwake na wenzake lakini alijua kwa vyovyote ndani ya ofisi hiyo anaweza kupata mwanga wowote. Aliwasili katika jengo la hazina saa mbili na dakika arobaini. Walinzi wa geti la upande wa nyuma hawakuwa na shida naye kwani ni mara nyingi walikuwa wakimwona akija katoka jengo hilo. Akawasalimia, nao wakamruhusu aendelee na shughuli zake.

Ofisi ilikuwa kimya kabisa, hata kama ingeanguka sindano basi ungeisikia. Akavuta hatua na kuwasha taa. Mwanga wa kutosha ukatawala chumba kile na kila kitu kikaonekana pasi na kificho. Jicho la Amata likatua moja kwa moja juu ya meza ya Madam S. mezani hapo palikuwa na karatasi nyeupe iliyoandikwa kwa kalamu nyekundu. Akavuta hatua na kuondoa kibweta cha wino kilichoikandamiza karatasi ile. Akaiinua na kuisoma kwa utulivu. Katika karatasi ile kukiandikwa maelezo mengi kwa kifupikifupi. Amata alijitahidi kuunganisha maelezo hayo ilia pate maana. Haikuwa kazi ndogo, lakini aliweza kufanikiwa kwa asilimia chache.

*Wizi wa 'Kokwa', Makumbusho ya Taifa, je hawa ndiyo wahusika?*

1. *Geofrey Kisinini – Mkurugenzi Mkuu???*
2. *Tabia Ismail – Afisa Maonesho ???*
3. *Kambale Kilonzo – Afisa usalama wa jengo???*

Taarifa ya kwanza aliweza kuielewa namna hiyo. Akayarudia yale majina mara tatutatu, hata mwenyewe hakujua kwanini anafanya hivo. Akaendelea kuunganisha vipande vya chini.

*Mpango umeanza kusukwa wapi?*

1. *Bahi Dodoma???*
2. *Mkuju Namtumbo???*
3. *Makumbusho ya Taifa Dar???*

Kisha Madam S alichora pembetatu na kuandika maeneo hayo matatu; Bahi, Namtumbo na Makumbusho ya Taifa.

Kamanda Amata akaigeuza nyuma ile karatasi na kukuta ujumbe mwingine.

*Kokwa ipatikane kwa udi na uvumba,*
*wahusika wakamatwe iwe jua iwe mvua.*

Pamoja nayo maelezo mengi sana yakafuatia ambayo Amata aliyaelewa vyema. *Je haiwezekani kuwa watu hawahawa ndiyo wamesababisha hiyo ajali? Na kama ndiyo basi kuna kiungo kati yao na serikali kwenye wizi huu… nani anayemjua Madam S na kazi yake kama si viongozi wachache ambao tunafanya nao kazi? Name naongeza maji yao hapa mmoja baada ya mwingine!* Amata akawaza na kwenye karatasi ileile akaandika majina ya watu wanne viongozi wa serikali ambao alihisi kuwa wanaweza kuwa na muunganiko na hili au kiungo kati ya wezi na serikali ili kuiba siri za huku kwenda kule. Si kwamba alikuwa na uhakika nao, la. Bali wao ndiyo haswa wanaofahamu kazi ya Madam S na ambao wangeweza kumuuza kiurahisi. Amaata aliikunja ile karatasi na kuitia mfukoni, kisha akaiacha ile ofisi na kuondoka zake.

Mwendo wa dakika kumi na mbili alifika yalipo makutano ya Barabara ya Samora na Mtaa wa Mirambo karibu kabisa na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM). Akatazama kwa makini yale mazingira. Ni hapa, kwa maelezo ya Gina ndipo Madam S alipopata ajali. Inasemekana gari hilo lilitokea upande wa Ocean Road likielekea Posta ya zamani lakini mara lilipomgonga likakunja kona kuelekea upande wa baharini. Aliyakumbuka haya maelezo kutoka kwa Gina. Katika kona ile Samora na Mirambo palikuwa na duka kubwa kwenye jengo la ghorofa tatu. Amata alilitazama eneo hilo kwa umakini sana na kukagua kwa nje kila

jengo lililo kwenye makutano hayo. Lengo lake kubwa ni kutaka kuona jengo lipi kati ya hayo lilikuwa na kamera za usalama zinazotazama barabarani. Kila jengo lililokuwa na kamera hizo, zote hazikutazama barabarani isipokuwa kwenye vibaraza vyake. Hizi aliona wazi hazitomsaidia sana. Alipokuwa katika uamuzi wa kuachana na hilo, wazo likamjia. *Ina maana Madam S alikuwa akitembea barabarani au kwenye korido za maduka?* Akatuliza akili. Akaanza upya uhakiki wa kamera zile na kuigundua moja ambayo kwayo aliona ingeweza kumsaidia. Hii ilifungwa kwenye moja ya duka ikitazama korido kwa uelekeo wa kuelekea Ocean Road. "Nitaanza na hii, usiku huuhuu" akajisemea na kumuendea mmoja wa walinzi waliokuwa eneo hilo.

"Habari bwana!" akamsalimu.

"Salama habari ya kazi," yule mgambo akamjibu Amata huku akivuta hatua kumkaribia, "Nikusaidie nini ndugu?" akauliza.

"Asante kwa ukarimu wako, mimi ni afisa wa polisi," Amata akajitambulisha na kumuonesha kitambulisho chake.

"Ndiyo afande nakusikiliza," yule mgambo akajibu na kuzima sigara iliyokuwa mkononi mwake kwa kusigina kwa mguu.

"Ikiwa namhitaji mwenye duka hili la kompyuta na vifaa vya elektroniki nampataje?" Amata akauliza.

"Bwana Patel?"

"Sijui anaitwa nani…"

"Patel… huyu bwana anaishi Kariakoo Mtaa wa India, na ametoka hapa muda si mrefu," yule mlinzi akaeleza.

"Una namba yake?" Amata akauliza.

“Ndiyo! Namba ya bosi wangu lazima niwe nayo,” yule mgambo akajibu huku akitoa simu yake. Ilikuwa simu ya kizamani iliyozungushiwa rubber-band. “Nimpigie?” akauliza.

“Ndiyo, mwambie kuna afisa wa polisi amekuja hapa anahitaji huduma dukani kwake,” Amata akampa maelekezo. Yule mgambo akapiga simu ile mara kadhaa haikupokelewa. Lakini baada ya dakika mbili hivi, simu ile ikaita. Patel alikuwa akipiga. Yule mgambo akaipokea simu ile na kuzungumza na bosi wake. Ilionekana wazi kuwa Patel alikuwa anaogopa maana Wahindi na polisi wanajuana wenyewe.

*“Yupo hapo sasa hivi?”* Amata aliisikia sauti ya Patel ikiongea baada ya yule mgambo kuweka sauti ya juu.

“Ndiyo yupo hapa, anasema usiogope uje ni jambo dogo tu!” yule mgambo akamwambia. Na simu ya Patel ikakatwa pasi na kutoa jibu lolote. Yule mgambo akajaribu kuipiga tena lakini haikuwa ikipokelewa kabisa. Dakika kumi baadae, Amata bado alikuwa eneo lile, liliwasili Land Cruiser jeusi na kuingia maegeshoni. Yule mgambo akamwambia Amata kuwa huyo aliyefika ni baba yake na Patel. Kweli, mlango ulipofunguliwa, waliteremka wanaume watatu. Wawili kati yao walikuwa watu wazima na mmoja alikuwa kijana kabisa. Walivuta hatua na kumfuata yule mgambo. Wakasalimiana.

“Yiko wapi bhana askari?” mmoja wao aliyeonekana mtu mzima aliyevalia kanzu aliuliza. Yule mgambo akwatambulisha kwa Amata. Wakasalimiana kisha wakamtaka Amata kuingia nao ndani ya lile jengo. Akawafuata.

***Itaendelea…***

**Tuandikie Whatsapp 0766974865**

**Tukupatie simulizi nyingine nyingi za kijasusi kwa bei nafuu kabisa!**